# Sehemu za Mpangilio wa Mpango wa P/CVE

Kuna sehemu kadhaa za mpangilio wa mpango ya P/CVE, na nyingi kati ya hizi sehemu za mpangilio zinaweza kutumika katika muktadha tofauti tofauti (mataifa, maeneo, jamii, n.k). Hata hivyo, unapopanga mradi wa P/CVE, shughuli zinazoangaziwa sharti ziongozwe moja kwa moja na muktadha maalumu wa mpango. Katika sehemu ifuatayo, tumegawanya shughuli za P/CVE katika makundi ya jumla. Kwa kila moja wa makundi haya, tunatoa mifano changanuzi ya shughuli maalum za P/CVE, ambazo mashirika yanaweza kutumia ili kutatua changamoto zao. Kwa kila mfano wa shughuli, tumeweka taarifa kuhusu miradi halisi inayotekelezwa na mashirika yakimaeneo kote duniani.

Kwa kuongezea mifano iliyoorodheshwa hapo chini, tunapendekeza rasilimali jumla zaidi kuhusu programu ya P/CVE:

- Hifadhidata ya CVE ya Uropa
- Mkusanyiko wa Makundi ya Uhamasishaji kuhusu Itikadi Kali
- Ofisi ya Mipango ya Mabadiliko ya Zana za CVE (USAID)

## Mbinu Zinazolenga Jamii

Mbinu ya kimaeneo unaoshughulikia mienendo mahususi na vichochezi vya itikadi kali za vurugu katika jamii iliyo katika hatari ya/au itikadi kali za vurugu inaweza kufaa katika kuzuia itikadi kali za vurugu, hasa kama itaendelezwa kwa muda. Ifuatayo ni orodha ya shughuli zinazoweza kutumika katika jamii.

| MAENEO YA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Elimu ya Uraia | Kusumbuliwa na serikali kwa mara nyingi hutambuliwa kama kichochezi cha itikadi kali za kivita. Kuna njia nyingi za kushughulikia suala hili, mojawapo ikiwa ni kuelimisha jamii kuhusu haki zao za uraia. Raia huenda hawajui haki zao za uraia na kile kilicho chao. Isitoshe, raia mara nyingi hawajui namna ya kufanya walio madarakani kuwajibikia makosa yao. Kwa kuwapa wanajamii elimu ya uraia ya msingi, wanapata ujuzi na maarifa yatakayowafanya waweze kuleta mabadiliko katika jamii zao. | Katika mwaka wa 2016, shirika la Union des Tunisiens Indépendants pour la Liberté (UTIL) ilizindua Muungano wa Elimu ya Raia wa Kiarabu. Kama sehemu ya mpango huu, UTIL ilitengeneza mwongozo wa matumizi ya elimu ya raia ili kuzuia na kukabiliana na itikadi kali za vurugu.<br><br>Katika mwaka wa 2019, Muungano wa Afrika Magharibi wa Kujenga Amani (WANEP) walitembelea UTIL mjiniTunis kujifunza kuhusu Mwongozo wa UTIL wa Elimu ya Raia. Katika kongamano hilo la kitaalam, UTIL na WANEP walijadili matumizi ya elimu ya raia katika kuzuia na kukabiliana na itikadi kali ya vurugu. Kisha UTIL ikasaidia WANEP kutumia Mwongozo wa Elimu ya Raia katika muktadha wa Mali.<br><br>Kenya Tuna Uwezo ni mradi unaofadhiliwa na shirika la USAID na unatekelezwa na shirika la Global Communities ambalo pia ulihusisha elimu ya raia. Kwa kushirikiana na washirika wa eneo husika, PeaceNet na Kituo Cha Sheria, mradi huo umewawezesha wakaazi hasa vijana kuwasilisha malalamishi yao na kutafuta suluhu kwa pamoja. |

| MAENEO YA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Utetezi wa jamii | Pamoja na elimu ya raia, kufundisha jamii jinsi ya kujitetea pia ni njia muhimu ya kukabiliana na itikadi kali. Mara nyingi, watu hujiunga na makundi ya itikadi kali kwa sababu wanahisi serikali zao hazitoi huduma muhimu na wananchi hawana uwezo wa kusema wanachotaka. Jamii zikifunzwa kupigania mahitaji yao kwa njia sahihi, ushawishi wa makundi ya itikadi kali utapungua. | Katika eneo la Diffa nchini Niger lililoathirika na itikadi kali za vurugu, USAID/OTI zilisaidia kuanzishwa kwa kundi la viongozi 12 wa jamii ili kujenga ustahimivu dhidi ya makundi ya itikadi kali katika maeneo yaliyoathiriwa na Boko Haram na ISIS- Africa Magharibi. Kundi hilo, Nalewa Mada ("Tunatafuta Amani"), kwa sasa linahusisha vijiji 30 viliyo na watu zaidi ya 300 wakiwemo vijana, kina mama, na viongozi wa kidini.<br><br>Mwaka wa 2017, muungano wa Neighborhoods Association IDMAJ uliandaa warsha ya siku tatu katika mji wa Casablanca nchini Morocco. Warsha hiyo ilihusisha watu 40 kutoka kwa mashirika ya umma, mashirika ya kiserikali, na taasisi za kidini na taasisi za elimu zilizoko maeneo yasiyopata huduma za kutosha katika eneo la Casablanca. Malengo ya warsha yalikuwa: (1) kufahamisha viongozi kutoka taasisi hizi kuhusu mashirika na makundi yenye misimamo mikali; (2) kujadili hatua za kuzuia uajiri kwenye makundi yenye itikadi kali, na (3) kutoa jukwaa la ushirikiano zaidi ili kukabiliana na uajiri. Miezi minne baadaye, IDMAJ ilifuatisha warsha ya pili na wawakilishi wa CSO, ili kubaini mbinu za usajili na mwitikio kuhusu itikadi kali katika kitongoji cha Sidi Moumen mjini Casablanca. Kwa mwelekezo wa IDMAJ, walioshiriki katika warsha waliunda vikundi vitano vya utetezi vinavyolenga jamii, ambavyo viliendelea kufanya kazi huko Sidi Moumen ili kuongeza viwango vya elimu na ufahamu kuhusu itikadi kali za vurugu. |
| Utumizi wa Mifumo ya Mtaa Kushirikisha Jamii | Mbinu zinazoongozwa na jamii na mifumo ya mitaa, imedhihirisha kuwa njia mwafaka ya kushirikisha wadau mbalimbali katika jamii. Kuwashirikisha wadau mbalimbali huwa muhimu katika kuelewa na kuzuia itikadi kali za vurugu. Kwa kutekeleza shughuli zinazoongozwa na jamii, uwezo wa wadau wenyeji huimarishwa, uwezo wao wa kukabiliana na itikadi kali za vurugu unaboreshwa, na ujasiri wa jamii dhidi ya itikadi kali unaimarika. | Mnamo mwaka wa 2019, Association Malienne Pour La Survie Au Sahel (AMSS) ulifadhili warsha za kuimarisha uthabiti na kutegemeana kati ya jamii mbili (Rharous na Séréré) katika eneo la Timbuktu, nchini Mali. Washirika katika warsha hiyo walijumuisha vijana, wanawake, viongozi waliochaguliwa, waandishi wa habari, machifu, viongozi wa kidini, wasimamizi na wawakilishi wa CSO. Katika kila warsha, AMSS ilitumia mbinu ya ushirikishaji wa washikadau mbalimbali (SCALE+) ili kubaini vitendo na mazoea yanayofaa kuimarisha ujasiri dhidi ya itikadi kali za kivita katika jamii hizi. Kisha AMSS ilisaidia wanajamii kutekeleza shughuli tatu za kuimarisha ujasiri wa jamii, zikiwemo: (1) msafara uliotumia mashindano ya michezo kueneza ufahamu kuhusu itikadi kali za vurugu miongoni mwa vijana; (2) warsha ya habari na uhamasishaji wa wanawake kuhusu jukumu lao katika kuzuia migogoro na itikadi kali za kivita katika jamii zao; na (3) warsha ya kuongeza uwezo wa vijana kushiriki katika mipango ya P/CVE.<br><br>*Nyenzo nyingine na/au miradi ya ushiriki wa jamii kulingana na mifumo ya ndani.*<br><br>• Jukumu la Jamii katika Kuzuia na Kukabili Misimamo Mikali ya Kivita inayosababisha Ugaidi (OSCE)<br>• Nafasi Salama Zana Zilizosasishwa za Kuwezesha Jamii na Kushughulikia Unyanyasaji wa Kiitikadi (Baraza la Masuala ya Umma la Waislamu)<br>• Ma3an,Tunisia (FHI 360)<br>• Sanad for Peacebuilding, Iraq (USIP) |
| Kubuni Sera ya Jamii | Usalama wa eneo wakati mwingine huwa tatizo katika jamii ambapo watu wanaweza kuathiriwa na hatari ya itikadi kali. Katika muktadha huu, kubuni mpango wa sera ya jamii ni njia mwafaka ya kushughulikia ukosefu wa usalama. Mipango ya sera ya jamii inalenga kuleta uhusiano mzuri kati ya polisi na jamii unaopelekea uaminifu na heshima. | Tathmini shirikishi ya vijana ya USAID iliyofanywa mwaka wa 2015 katika Tangier na Tetouan nchini Morocco, ilifichua kuwa ukosefu wa usalama kwa vijana katika vitongoji vyao unaweza kuhusishwa na ukosefu wa polisi. Ili kuimarisha ushiriki wa kidemokrasia, Serikali ya Morocco ilifanya msururu wa mageuzi ambayo yaliupa kipaumbele ushirikiano wa moja kwa moja kati ya polisi, mamlaka za mitaa na raia ili kukabiliana vyema na mahitaji yao na kuboresha ufanisi wa polisi. USAID inaunga mkono juhudi za mageuzi za serikali kupitia mradi wa majaribio ya Shughuli ya Sera ya Jamii (COPA). Kabla ya mradi huu, wakaazi vitongojini hawakuzungumzia usalama wao kwa uwazi. Kupitia kwa COPA, jamaa hao hao wametupilia mbali tofauti zao na kujifunza ujuzi mpya unaosaidia kuboresha usalama katika jamii zao. USAID inaboresha ujuzi wa polisi na wakaazi ili kuwasaidia kushirikiana katika kukabiliana na masuala ya usalama.<br><br>*Rasilimali zingine muhimu na/au mipango kuhusu sera ya jamii:*<br><br>• Kuzuia Ugaidi na Kukabiliana na Misimamo Mikali na Itikadi Kali za Kivita zinazosababisha Ugaidi: Mbinu ya Sera ya Jamii (OSCE)<br>• Mbinu ya Sera ya Jamii nchini Bangladesh (The Asia Foundation)<br>• Mbinu ya Sera ya Jamii kwa Timor-Leste (The Asia Foundation) |

| MAENEO YA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Mkakati wa Jamii ili Kuzuia Itikadi Kali za Kivita | Unapotumia mbinu ya msingi ya mifumo ya ndani ili kuzuia itikadi kali za kivita, hatua ya kwanza ya kawaida ni kukusanya wanajamii na kuweka mkakati wa jamii. Kwa kujumuisha usemi wa jamii, changamoto zao, na suluhisho wanazopendekeza, itakuwa ya manufaa sana kwa jamii. Kwa kuanza na mbinu inayoongozwa na jamii, uwezekano wa jamii kukubaliana na mpango wa kuzuia itikadi kali za kivita unaongezeka, na kuchangia katika kufanikisha matokeo mazuri ya mpango huo. | Shughuli ya Kenya NiWajibu Wetu (NIWETU), zinazofadhiliwa na USAID na kutekelezwa na DAI, zinaimarisha uwezo wa CSO na washawishi wa jamii ili kuongoza miradi ya CVE. Tangu mwaka wa 2016, NIWETU imeshirikiana na mashirika 39 nchini, kupanga shughuli mahususi zinazoambatana na muktadha mahususi kote nchini. NIWETU pia inafadhili mabingwa 52 wa mabadiliko ya CVE (C4Cs) katika kaunti tano nchini Kenya kupitia mafunzo, ushauri na usaidizi endelevu wa kiufundi.<br><br>Katika mwaka wa 2016, Association Chifae, iliandaa mafunzo ya siku mbili kwa watafiti 52, wanaharakati wa mashirika ya kijamii, mamlaka ya umma, polisi, na wanahabari ili kubuni mikakati ya kuzuia na kukabiliana na itikadi kali zinazosababisha itikadi kali za vurugu katika eneo la Tangier, Morocco. Kutokana na pengo la kutoelewa vichochezi vya itikadi kali za kivita katika eneo la Tangier, pamoja na ukosefu wa suluhisho thabiti la kukabiliana na suala hilo, mafunzo hayo yaliimarisha uwezo wa wadau wa ndani kuongeza ufanisi na matokeo ya miradi yao ya kuzuia itikadi kali za vurugu.<br><br>*Nyenzo nyingine muhimu na/au miradi ya ushiriki wa wadau katika jamii:*<br><br>• Kukuza Mbinu Inayoongozwa na Jamii katika Kukabili Itikadi Kali za Kivita (Shirika la Dunia la Maendeleo ya Rasilimali na Elimu) |
| Kuimarisha Uwezo wa Viongozi wa Mitaa kuhusu Kukabiliana na Itikadi Kali za Kivita (CVE) | Kubuni mbinu inayolenga jamii kunaweza kuhusisha kujenga ushirikiano na kuimarisha uwezo wa viongozi wa jamii kama vile viongozi wa manispaa, viongozi wa kidini, wazee wa kijiji au watu wengine wenye ushawishi katika jamii. Viongozi hawa wanapaswa kumiliki viwango tofauti vya mamlaka na ushawishi, iwe kiongozi aliyechaguliwa rasmi au kiongozi mheshimika ambaye hajachaguliwa rasmi. Viongozi hawa wanaweza kuwa washirika muhimu katika jamii na wanaweza kuongeza matokeo za shughuli za P/CVE. | Mnamo mwaka wa 2016, Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ilipa ICMA pesa ya Kujenga Utaalamu wa CVE kwa Mamlaka za Manispaa eneo la Magharibi ya Balkans, mradi uliobuniwa kukuza ushirikiano kati ya serikali, mashirika ya kiraia na sekta ya kibinafsi ili kuongeza ushirikiano na jamii na ustahimilivu dhidi ya itikadi kali. Mradi huo ulipania kuunganisha, kutoa mafunzo, na kuwahamasisha mameya na viongozi wa manispaa katika eneo lote la Balkans Magharibi, ili kutambua na kushughulikia mambo hatari yanayoambatana na itikadi kali za kivita kupitia kushirikiana na Strong Cities Network. Kundi linalosimamia mradi lilifanya ziara ya uhamasishaji iliyohusisha mikutano 85 na kuzihusisha serikali 58 za mitaa. Walipanga warsha ya kuimarisha uwezo wa watu 236 katika nchi nne kati ya sita zinazolengwa, na kuandaa mkutano wa mwisho wa kikanda unaolenga manispaa ya mataifa yote sita, na uliohudhuriwa na watu 107 kutoka kwa serikali 28 za mitaa. Utafiti wa kabla na baada ya warsha ulionyesha kuongezeka kwa ujuzi wa CVE na ujasiri wa kuchangia juhudi za kitaifa na kimataifa za kukabiliana na msimamo mkali wa kivita. |

## Vyombo vya habari na Mawasiliano

Njia ya kawaida sana ya kushughulikia itikadi kali za kivita ni kupitia kwa vyombo vya habari na mawasiliano. Kuna aina mbalimbali za vyombo vya habari na vyenzo vya teknolojia vinavyoweza kutumika kwa masuala ya mawasiliano, na kila mojawapo inapaswa kubinafsishwa kwa kila mbinu ya utekelezaji wa itikadi kali za kivita. Lengo la shughuli hizi ni kukuza usemi wa viongozi wa kadri, kueneza usemi mbadala kwa walengwa wa washirika yenye itikadi kali za kivita, kupuuza usemi wa mashirika ya itikadi kali ya kivita, na/au kuendesha mazungumzo miongoni mwa jamii zenye tamaduni tofautitofauti. Ifuatayo ni mifano ya shughuli zinazoweza kutegemea mawasiliano ambazo zinaweza kutumika kwa P/CVE.

| MAENEO YA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Kukuza Usemi wa watu wenye viwango vya kadri | Mipango mingi ya mawasiliano hupania kujenga ustahimilivu dhidi ya ushawishi wa itikadi kali miongoni mwa jamii. Mojawapo wa mbinu za kufanikisha ushawishi huo ni kukuza usemi wa watu wa viwango vya kadri katika maeneo yaliyo katika hatari ya itikadi kali za kivita. | Mradi wa Somali Voices nchini Kenya, ulioanzishwa na Equal Access unalenga jamii ya Waislamu katika kaunti za Nairobi, Wajir, Garissa Kaskazini na Mashariki mwa Kenya. Mradi huu unaimarisha uwezo wa washawishi wakuu wa jamii, wakiwemo vijana, wazee, viongozi wa kidini na viongozi wa wanawake ili kujenga uwezo wa jamii kukabiliana na ujumbe wenye itikadi kali na kubuni jumbe bunifu na kampeni za kuhamasisha jamii.<br><br>Mifano mingine:<br><br>• Mradi waVoices for Peace katika Afrika Magharibi |

| MAENEO YA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Simulizi mbadala | Tofauti na kupinga ujumbe wenye itikadi kali moja kwa moja, simulizi mbadala inawasilisha njia mbadala ya kushughulikia ujumbe wa misimamo mikali. Nyenzo nyingi za mawasiliano zinaweza kutumika kusambaza simulizi mbadala, na mara nyingi huwa na ufanisi zaidi kutumia mchanganyiko wa zana (k.m., Televisheni, redio, Facebook, Ujumbe mfupi), ikiwa ni pamoja na zana zinazotumiwa na VEO kufikia hadhira inayolengwa. | Salam Shabab ni kipindi maarufu cha televisheni cha kuleta amani miongoni mwa vijana nchini Iraq. Kulingana na mtaala wa elimu, msururu huu wa vipindi vya televisheni uliwaleta pamoja vijana wa Iraq ili kushindana katika mashindano manne ikiwemo filamu fupi, michezo, mashindano ya kiakili na katika ukumbi wa michezo. Timu iliyoshinda iliwakilisha vijana kutoka sehemu mbalimbali za nchi, na kuwahimiza kufanya kazi pamoja ili kuibuka na ushindi. Kwa kufanya hivyo, walitoa mfano mzuri kwa vijana wanaotazama televisheni. Msururu huo wa vipindi uliopeperushwa kwenye chaneli nyingi za televisheni nchini Iraq kuanzia 2009-2013 uliwashirikisha vijana kote Mashariki ya Kati kwenye mitandao ya kijamii na ukajenga ustahimilivu miongoni mwa vijana katika kukabiliana na migogoro na itikadi kali.<br>Mifano mingine:<br>• Ourmindanow Alternative Messaging Hub nchini Ufilipino<br>• Mpango waWhite Dove katika eneo la Kaskazini mwa Nigeria na Bonde La Ziwa Chad<br>• Mpango waHirka Nabadda nchini Somalia<br>• Mpango waOne Village, A Thousand Voices nchini Afghanistan |
| Kukabiliana na Semi za itikadi kali | Kuzuia uenezaji wa jumbe za itikadi kali za kivita linaweza kutazamwa kama neno la jumla linaloashiria shughuli zote za mazungumzo ya kupambana na jumbe za itikadi kali, ikiwemo usemi mbadala. Hata hivyo, jumbe za kupinga mara nyingi humaanisha kuangazia moja kwa moja na kukanusha ujumbe ulioko ambao unaeneza itikadi kali. | Mradi wa BRAVE project nchini Kenya unahamasisha viongozi wa kidini na wanajamii wengine kuunda mfumo wa kupinga na kupambana na jumbe za itikadi kali. Kwa kufanya kazi na viongozi wa Kiislamu, Kikristo na wa madhehebu mbalimbali, mradi huo ulitoa mafunzo na vifaa vya kazi kwa makundi ya kidini kuhusu jinsi ya kukabiliana na ujumbe wenye misimamo mikali mtandaoni kwa kurejelea tafsiri za wastani za vitabu vya dini.<br>Mifano Mingine:<br>• Mradi wa #NotAnotherBrother nchini Syria<br>• Mradi wa Burka Avenger nchini Pakistan<br>• Iman movie trailer nchini Sudan |
| Mawasiliano kuhusu Mabadiliko ya Kijamii na Tabia (SBCC) | SBCC ni kimkakati ya matumizi ya mbinu za mawasiliano ili kukuza mabadiliko ya maarifa, mitazamo, kanuni, imani, na tabia. Hii inaweza kutumika katika sekta nyingi, ikiwemo afya ya umma, elimu na P/CVE. | Nchini Morocco, Association Chifae ulibaini kwamba kuelimisha, kufahamisha na kuongeza ufahamu miongoni mwa wazazi na wale wanaohusika katika elimu ya kijamii hakutoshi kuhamasisha jamii na vijana katika vita dhidi ya VE. Chifae uliwafunza wafanyikazi wa kijamii na walimu kuhusu mbinu za mawasiliano ya kijamii na kisha ukafanya kampeni ya kuongeza ufahamu kuhusu itikadi kali miongoni mwa watu huko Beni Makkada.<br>Mifano mingine:<br>• The Team (Kenya, Tanzania, Indonesia) |
| Mazungumzo Baina ya Tamaduni mbalimbali | Kuwezesha mazungumzo baina ya tamaduni tofauti ni njia mwafaka ya kujenga uvumilivu na uaminifu kati ya makundi, hali ambayo huimarisha uwiano na ustahimilivu wa jamii dhidi ya VE. Mazungumzo pia yanaweza kutumika kati ya haya makundi kutambua nafasi za ushirikiano miongoni mwa jamii zao. Mazungumzo haya hasa ni muhimu katika jamii ambamo migawanyiko kati ya makundi unatumiwa vibaya na makundi yenye itikadi kali. | Kupitia kwa Mradi wa Peace through Development Project, muungano wa pour la Dialogue entre les Jeunes des Diverses Religions (ADJR) nchini Chad, ulifanya mijadala baina ya dini mbalimbali ili kuleta vijana mbalimbali pamoja. Washiriki walijifunza jinsi ya kusaidia kuwezesha mazungumzo baina ya dini mbalimbali katika jamii zao. Mwishoni mwa kila mazungumzo, ADJR ilienda mikoani ili kushiriki maarifa waliopata na jamii zao pana. Washiriki kutoka kila mkoa pia walibuni mipango ya kusambaza ujumbe mbadala katika jamii zao, ikiwemo kupitia vipindi vya redio, mijadala shuleni na ukumbi wa michezo. Kwa mfano, vijana washiriki walitembelea shule kadhaa kujadili uvumilivu, kuishi kwa amani na vurugu shuleni.<br>Mifano mingine:<br>• Mpango wa Kuleta aAmani nchini Yemen |

## Raslimali za Ziada Kuhusu Vyombo vya Habari na Mawasiliano ya P/CVE:

- Maktaba ya Kupinga Semi (Kituo cha Hedayah)
- Kitabu cha Kupinga Semi (Kituo cha Mazungumzo ya Kimkakati)

## Elimu

Mnamo Desemba 2015, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa alitoa Mpango wa Utekelezaji wa Kuzuia itikadi kali, ambao ulitaka kuwepo kwa mbinu ya kina ya kushughulikia hali za kimsingi zinazowafanya watu kuwa na itikadi kali za vurugu. Kwenye mpango huo, Umoja wa Mataifa ulisisitiza sana kuhusu elimu, kwa sababu elimu inaweza kutumika kwa njia nyingi kukabiliana na itikadi kali. Ifuatayo ni baadhi ya mifano.

| ENEO LA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Kufikiri kwa Makini na Kujenga Ujuzi | Ukosefu wa uwezo wa kufikiria kwa makini na ujuzi husika, unaweza kuwafanya vijana rahisi kuathiriwa na itikadi kali. Mipango inayolenga kujenga ustahimivu dhidi ya itikadi kali kwa njia ya elimu inakuza kufikiria kwa makini na ujuzi mwingine, unaweza kusaidia kuzuia hii hatari. | Kukiwa na takriban nusu ya wakaazi wa Mali walio chini ya umri wa miaka 18, na zaidi ya asilimia 15% ya ukosefu wa ajira kwa vijana, vijana wa Mali wana fursa chache za kazi yenye maana. Viwango vya juu vya ukosefu wa elimu miongoni mwa vijana na ukosefu wa ajira husababisha uhamiaji na chuki kwa ujumla. EDC ilisaidia vijana wa vijijini nchini Mali kukuza ujuzi wao kupitia PAJE-Nièta (Projet d'Appui aux Jeunes Entrepreneurs), au mradi wa Mali wa Vijana Walioondoka Shuleni. EDC ilifanya kazi na vijana katika maeneo ya vijijini ili kuwasaidia kupata elimu bora, kuwa na tija ya kiuchumi, na kujihusisha katika masuala ya raia. |
| Elimu ya Amani | Pamoja na kujumuisha maudhui ya P/CVE katika mitaala ya elimu ya kitaifa, mipango inayolenga elimu ya amani pia inaweza kusaidia kukabiliana na itikadi kali. Katika jamii ambapo kuna migogoro ya kivita, elimu ya amani inaweza kupunguza mivutano. Mipango ya elimu ya amani kwa kawaida huzingatia stadi za kimaisha kama vile mazungumzo, kutatua matatizo, na kusikiliza kwa makini ili washiriki waweze kutumia matukio katika maisha yao ya kila siku, ikiwemo kukabiliana na watu wenye itikadi kali. | Tangu 2014, USIP imefanya kazi kwa karibu na taasisi nchini Afghanistan kukuza Elimu ya Amani. USIP ilianza kufanya kazi na vyuo vikuu vya umma na vya kibinafsi na Wizara ya Elimu ya Juu ya Afghanistan (MoHE), ili kuandaa mtaala wa masomo ya amani na migogoro unaoweza kufundishwa na vyuo vikuu kote nchini. Zaidi ya hayo, USIP iliongoza wanafunzi na kitivo katika vyuo vikuu washirika kuunda vilabu vya amani ambavyo vinashirikisha wanafunzi kuhusu masuala na shughuli zinazojenga umoja na mahusiano ya amani kati ya jamii mbalimbali za chuo. Mwaka wa 2015, USIP ilishirikiana na Help the Afghan Children (HTAC), kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Elimu ya Afghanistan, kuandaa mtaala wa elimu ya amani kwa darasa la 7-12. HTAC imetoa mafunzo kwa walimu 1,800 kutoka vyuo sita vya ualimu katika mikoa ya Parwan, Kabul na Nangarhar ili wafunze elimu ya amani. |
| Kushirikiana na Taasisi za Elimu ya Kidini | Katika jamii nyingi, elimu ya kidini ni sehemu ya msingi ya mtaala wa elimu. Nyakati nyingine, elimu ya kidini ndiyo ya msingi au chanzo pekee cha elimu. Katika jamii kama hizo, kushirikiana na taasisi za elimu za kidini inaweza kuwa njia mwafaka ya kupambana na itikadi kali. Isitoshe, kupitia ushirikiano huu, mipango inaweza kuondoa mawazo ya kawaida kwamba itikadi kali zinaambatana na dini, huku zikiendeleza hoja kwamba taasisi za kidini zinaweza kuwa na ushawishi sana katika kuzuia itikadi kali. | Vijana wengi waliotatizika nchini Chad wanasoma katika shule za Qur'ani badala ya shule za sekta rasmi ya elimu. Kwa usaidizi kutoka kwa Ubalozi wa Marekani mjini N'Djamena, Taasisi ya Salam ilitekeleza mradi waKuhimiza Maadili ya Kiraia na Elimu ya Maingiliano Katika Shule za Kurani za Chad ambao ulilenga kuimarisha vituo vya maisha ya jamii na ustahimilivu. Mradi huu uliwashirikisha viongozi maarufu kama vile walimu wa shule za Qur'ani ambao wana ushawishi mkubwa zaidi kwa vijana waliotengwa kutoka kwa jamii zinazoathiriwa zaidi na vichochezi vya itikadi kali vya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Taasisi ya Salam ilitoa mafunzo na usaidizi wa kiufundi kwa kufuatilia zaidi ya walimu 200 wa shule za Qur'ani katika maeneo kumi.<br>*Rasilimali na/au mipango zingine za kushirikiana na taasisi za elimu ya kidini:*<br>• Kukuza Elimu ya Amani katika Shule za Islamiya (Tahadhari ya Kimataifa)<br>• Shirika la SCORE nchini Kenya |

### Raslimali zaidi kuhusu Elimu na P/CVE:

- Mbinu Zinazoibuka katika Usanifu, Ufuatiliaji na Tathmini ya Elimu kwa Mipango ya Kujenga Amani (Tafuta Maridhinao)
- Warsha ya Kujenga Uwezo wa Kitaifa kuhusu Kuzuia Misimamo mikali ya Ukatili Kupitia Elimu nchini Uganda (Hedayah)
- Mwongozo Unaoongozwa na Vijana juu ya Kuzuia Misimamo Mikali ya Ukatili Kupitia Elimu (UNESCO)
- Kuzuia Itikadi Kali za Ukatili Kupitia Elimu: Mwongozo kwa Watunga Sera (UNESCO)
- Mwongozo wa Mwalimu wa Kuzuia Misimamo Mikali (UNESCO)
- Uzuiaji wa Itikadi Kali Zinazohimiza Matendo ya Vurugu Utangulizi wa Elimu na Uzuiaji wa Itikadi Kali zinazohimiza Matendo ya Vurugu (Mtandao wa Wakala wa Elimu kwa Wakati wa Dharura)

## Kuwashirikisha Washawishi

Unapokabiliana kuzuia au kukabiliana na itikadi kali za kikatili, uhusishaji wa watu ambao wana ushawishi inaweza kuwa mbinu mwafaka. Washawishi wanaweza kuwa wanafamilia, wanajamii, wanarika, au hata watu wanaojulikana sana. Washawishi mara nyingi wanaweza kusaidia kubadilisha mitazamo au kufanya maamuzi kwa niaba ya wale wanaozingatia itikadi kali za kikatili. Kuna njia nyingi za kuwashirikisha washawishi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano.

| ENEO LA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Kushirikisha Wanafamilia | Mara nyingi, huwa muhimu kuwashirikisha wanafamilia katika kukabiliana na itikadi kali za vurugu. Ushirikisho huo unaweza kuhusu uelimishaji wa wazazi kuhusu visababishi vya itikadi kali ya kikatili miongoni mwa vijana na kuwafundisha wazazi kutambua dalili za itikadi kali na jinsi ya kuwasiliana na watoto wao. Njia nyingine ni kuweka raslimali za jamii kwa wanafamilia, kama vile simu ya dharura au kikundi cha usaidizi ambapo wanaweza kueleza wasiwasi wao ikiwa wanamjua mtu anayejiunga na itikadi kali za kikatili. | Shirika la Women without Borders (WwB) lilianzisha wazo la kina mama kuzuia itikadi kali za ukatili (MPVE) kupitia kwa mradi wa SAVE network mwaka wa 2008. WwB ilianzisha na kurasimu MotherSchools: Mtindo wa Parenting for Peace. Mbinu hii ya uzuiaji wa chini kwenda juu inatoa kipaumbele kwa usalama wa kina mama husika walio katika jamii zilizoathirika. Mtaala huu unaimarisha uwezo wa kibinafsi wa wanawake, uwezo, na elimu ya kihisia, na huongeza ufahamu wao kuhusu ushawishi wa itikadi kali. WwB imerekebisha programu na imeshirikisha zaidi ya akina mama elfu mbili katika nchi kumi na mbili kote Ulaya Magharibi na Mashariki; Asia ya Kati, Kusini na Kusini-mashariki; Mashariki ya Kati; na Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. MotherSchools pia huboresha huduma zilizopo za kijamii na uwezo wa ndani kwa kuwapa wadau wa mashirika ya kiraia katika maeneo hatari miundo muhimu, zana, na ujuzi wa kukabiliana na itikadi kali.<br>Mifano mingine:<br>• Familia Dhidi ya Ugaidi na Misimamo Mikali (ulimwenguni) |
| Kuwashirikisha Wadau wa Kdini | Watu binafsi wanaweza kuvutiwa na vuguvugu la itikadi kali kwa sababu nyingi. Sababu moja ya kawaida ni kutafuta usafi wa kiroho, nidhamu au hamu ya kuwa sehemu ya kitu kikubwa zaidi. Viongozi wa kidini kwa kawaida ni wanajamii wanaoheshimika na mara nyingi huwa na ushawishi wa hali ya juu kwa wafuasi wao. Kama matokeo, viongozi wa kidini ni washirika wazuri katika mipango ya kuzuia au kubadilisha itikadi kali. | Mradi wa 1 Sadaqa 1 2 2 ulifanya kazi na Wizara ya Masuala ya Kiislamu (MoIA) kukuza amani na ustahimilifu nchini Mauritania kwa kuimarisha uwezo muhimu unaohitajika kukabiliana na itikadi kali za kivita. Shughuli hii ya majaribio ilishirikiana na MoIA kuunda mkakati na mbinu za kusaidia jamii ambazo vijana wako katika hatari kubwa zaidi ya kuajiriwa na VEO. Mradi huo uliipa MoIA ujuzi wa kuwezesha mabaraza ya umma, usuluhisho wa migogoro, kuwashirikisha vijana, kubaini sababu za hatari za itikadi kali na vyombo vya habari na mawasiliano. Kisha mradi ulifanikisha MoIA katika kutumia ujuzi huu kukabiliana na itikadi kali kwa kushirikiana na washikadau tofauti. Kutokana na hilo, MoIA iliweza kufikia kubwa na kuboresha uwezo wake wa kufanya kazi kwa ufanisi na viongozi wa kidini na wa jamii ili kukuza amani na ujasiri.<br>*Nyenzo nyingine na/au mipango ya kuwashirikisha watendaji wa kidini:*<br>• Kushirikisha Dini na Vyombo vya Kidini katika Kukabiliana na Itikadi kali (USIP)<br>• Kituo cha Upatanishi wa Dini Mbalimbali (Nigeria) |

## Shughuli za P/CVE zinazolenga jinsia

Ingawa miradi ya P/CVE mara nyingi inasisitiza jukumu la wanaume, wanawake pia wanaweza kuwa washiriki wachangamfu katika masuala ya itikadi kali. Wanaweza kuwa waajiri, waungaji mkono, na wapiganaji, lakini wanaweza pia kuwa wazuri sana kama wajenzi wa amani na viongozi katika kuzuia migogoro. Shughuli za P/CVE lazima zitofautishe kati ya mahitaji na vipaumbele vya vijana wa kike na wa kiume ili kuunda fursa ambazo zitaongeza uwezo na michango yao. Ili kuzuia mvuto kwa itikadi kali miongoni mwa wanawake, shughuli mbalimbali mahususi za kijinsia zinawezeza kuidhinishwa. Zifuatazo ni baadhi ya mifano:

| ENEO LA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Shirikisha Wanawake na Wasichana kama Washawishi | Wanawake ni washiriki muhimu katika juhudi za P/CVE za ndani kwa kuwa wana ujuzi na ushawishi muhimu katika jamii na familia zao. Hivyo basi, mara nyingi wanawake wana nafasi nzuri zaidi ya kutambua dalili za itikadi kali na kukanya itikadi kali za vurugu kwenye familia zao. Wanaweza pia kuwa muhimu katika kuhamasisha, kujenga uwezo miongoni mwa wanawake wengine katika eneo lao – hivyo kuweza kuzidisha nguvu ya kupigana na itikadi kali katika jamii ambapo kuna uwezekano wa kusajiliwa kwenye itikadi kali. | Mradi wa Kupigana na Itikadi Kali katika Kawar Maila unalenga kubuni suluhu ya kibunifu inayolenga kukabiliana na itikadi kali Kaskazini Mashariki mwa Nigeria, ambayo imekumbwa na viwango vya juu vya kuajiriwa na Boko Haram. Mradi huo unafanya kazi kusaidia uongozi wa wanawake katika kukuza haki, amani na usalama wa binadamu na unatarajia kuongeza uongozi wa wanawake, kutoa jukwaa la mafunzo kati ya mashirika ya kiraia ya mitaa, Mashirika Yasiyo ya Serikali na washirika wa serikali, na pia kati ya wanaharakati wa chini nchini Nigeria na katika nchi jirani.<br>Mifano mingine:<br>• Empowered Women, Peaceful Communities (UN Women)<br>• STRIVE (Royal United Services Institute) |
| Kukuza Haki za Kibinadamu na Usawa wa Wanawake na Wasichana | Kukuza na kulinda haki za binadamu za wanawake na wasichana ni sehemu muhimu ya kuzuia itikadi kali za kikatili. Ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya wanawake na wasichana mara nyingi hushamiri katika jamii zilizo na viwango vya juu vya kuajiriwa na makundi yenye itikadi kali. Kwa kufanya kazi ili kuzuia unyanyasaji siku zijazo, itapunguza wanawake kujiunga na makundi ya itikadi kali. Kwa kuwawezesha wanawake katika jamii, kunaongeza uwezo wao wa kufanya shughuli za P/CVE na kuwa washawishi wema katika jamii zao. | Mnamo mwaka wa 2016, Search for Common Ground ilishirikiana na Rabita Mohammadia wa Ulemas, kutekeleza mradi wa Women's Caravan for Peace ambao ulihusisha midahalo iliyoongozwa na mashirika ya kijamii na wanachama wa watu wasiojiweza Kaskazini mwa Morocco, pamoja na miji ya Nador, Al Hoceima, Tétouan na Tangier.. Shughuli hizo ziliongeza ustahimilivu, uhuru wa fikra, utatuzi wa migogoro na haki za wanawake. Mradi huo ulitambua kuwa ili kukabiliana na uharibifu unaoletwa na jumbe za itikadi kali, ni vyema kubuni njia zuizi zinazolenga visababishi vya itikadi kali.<br>Mifano mingine:<br>• MotherSchools: Parenting for Peace (Women Without Borders) |
| Kuwawezesha Wanawake na Wasichana Kiuchumi | Mojawapo wa vishawishi vya imani za itikadi kali ni umaskini. Baadhi ya mbinu za mafanikio za kujenga ustahimilivu dhidi ya itikadi kali, hasa miongoni mwa wanawake ni kupitia kwa uwezeshaji wa kiuchumi. Sauti ya wanawake ikiweza kusikika sana katika jamii kupitia kwa ongezeko la fursa za uchumi (k.m., mikopo midogo), wanaweza kuzuia makundi yanayotaka kuwaajiri wanajamii wao. | Katika kukabiliana na mashambulizi ya kigaidi nchini Bangladesh mwaka 2005, serikali haikusasisha tu mkakati wake wa CT/CVE ili kujumuisha kukabiliana kwake na masuala ya usalama, lakini pia ilijumuisha kipengele cha uwezeshaji kiuchumi kwa wanawake. Hii ni pamoja na utoaji wa mikopo midogo midogo kwa wanawake, kuongeza mahudhurio ya shule za msingi kwa wasichana na kuongeza kazi za kiwanda cha nguo kwa wanawake. Kupitia kwa elimu na fursa zaidi za kiuchumi, wanawake na wasichana wana njia mbadala badala ya kuunga mkono na kuhusika katika mashirika yenye itikadi kali.<br>Mifano mingine:<br>• Sisters Without Borders (Women in International Security)<br>• Let's Live in Peace (Paiman Alumni Trust) |

## Rasilimali zaidi kuhusu Uwezeshaji wa Wanawake:

- Mbinu za Kijinsia Za Kukabiliana na Itikadi Kali: Mafunzo Kutoka kwa Wanawake Wanaohusika na Ujenzi wa Amani na Kuzuia Vurugu Yaliyotumika na kuwa na Mafanikio nchini Bangladesh na Morocco (Brookings)
- Jinsia na Mitazamo ya Kimtadha katika Kukabiliana na itikadi kali ya kikatili (CVE).Kuchunguza Ujumuishaji wa Wanawake na Mambo ya Muktadha katika Mbinu za Mtandaoni za CVE
- Mazoea Mazuri kwa Wanawake na Kukabiliana na Misimamo Mikali ya Kikatili (GCTF)
- WANAWAKE NA ITIKADI KALI ZA KIVITA: USHIRIKA WA WANAWAKE NA WASICHANA WENYE VIKUNDI VYA JIHADI NA ATHARI ZA UPANGAJI (DFID)
- Wanawake na Itikadi za Kikatili nchini Jordan (UN WOMEN)
- Kuelewa Nafasi ya Jinsia katika Kuzuia na Kukabiliana na Misimamo Mikali Inayosababisha Ugaidi (OSCE)
- Kuimarisha Nafasi ya Wanawake katika Kuzuia na Kukabiliana na Itikadi Kali za Kikatili (Women Without Borders)

## Sera na Utafiti

Kando na kufanya shughuli za P/CVE za ana kwa ana katika jamii za eneo husika, mashirika yanaweza pia kufanya utafiti wa P/CVE na kutoa mwongozo wa sera. Ifuatayo ni mifano ya baadhi ya shughuli hizo.

| ENEO LA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Mikakati ya P/CVE ya Kitaifa (na nchi/kaunti) | Katika miaka ya hivi karibuni, mataifa mengi yameshughulika na kubuni mikakati ya kitaifa ya P/CVE kusaidia kupunguza itikadi kali. Kila mikakati ni wa kipekee kwa kila nchi, lakini nyingi kati ya hizo inashughulikia masuala yanayopelekea kwa/au kuzuia itikadi kali za kigaidi. Baadhi ya nchi, kama vile Kenya, zimebuni mikakati ya P/CVE ya kiwango cha kaunti ili kutoa mwelekeo unaolenga vitisho vya kieneo. | Mataifa kadhaa yamebuni mikakati ya P/CVE au yamejumuisha mkakati katika Mipango yao ya Kitaifa ya Utekelezaji. Kwa kiungo cha kufikia mikakati ya haya mataifa, tafadhali ona tafadhali angalia Kiambatisho 1 cha Hedayah Miongozo na Matendo Mema: Kukuza Mikakati ya Kitaifa ya P/CVE na Mipango ya Utekelezaji.<br><br>Nchini Kenya, mpango wa NIWETU umekitwa katika Mkakati wa Kitaifa wa Kenya wa Kukabiliana na Itikadi Kali na imekuwa ikitumika katika ngazi ya kaunti kuanzisha mipango ya utekelezaji ya P/CVE katika kaunti zilizo hatarini kama Kwale na Mombasa.<br><br>*Nyenzo muhimu kwenye mikakati ya kitaifa ya P/CVE:*<br>• Mikakati ya Kitaifa ya CVE (Hedayah) |
| Tathmini ya P/CVE | Utathmini wa VE ni mbinu ya kawaida ya utafiti ya kuelewa vichochezi vya itikadi kali katika muktadha maalum. Kutathmini kwanza kabla ya kutekeleza shughuli kunaweza kufichua mienendo muhimu ya eneo la VE. Kisha taarifa hii inaweza kuingia moja kwa moja kwa muundo na utekelezaji wa shughuli zingine za P/CVE. | Mnamo mwaka wa 2016, Association Malienne Pour La Survie Au Sahel (AMSS) kilifanya uchunguzi ili kubaini masuala yanayopelekea itikadi kali (VE), nchini Mali. Utafiti ulijumuisha tafiti fupi, vikundi lengwa na mahojiano muhimu. Utafiti ulifanywa katika jamii tano tofauti - Tombouctou, Goundam, Diré, Niafunké na Rharous – zote zikiwa eneo la Tombouctou. Kutokana na utafiti katika kila eneo, AMSS ilifadhili kongamano na wadau ili kushiriki, kusambaza na kujadili na kudhibitisha matokeo. Wahusika walihusisha viongozi wa serikali, viongozi wa CSO, na wanajamii.<br><br>Mifano mingine:<br>• Ustahimilivu wa Jamii kwa Itikadi Kali nchini Kenya (USIP)<br>• Vichochezi vya Kujiunga na Makundi ya Itikadi Kali za Kikatili nchini Kosovo (ICSVE)<br>• Je, Jordan iko kwenye Hatari gani za Itikadi Kali? (IRI) |

## Urekebishaji na Kukubaliwa Tena katika Jamii

Kurekebisha na kujiunga tena katika jamii (R&R) kwa waliojiunga na makundi ya itikadi kali ni kipaumbele cha serikali yote duniani. R&R inaendelea kuwa kupaumbele cha kila jamii ambayo imeathiriwa na kurudi kwa wapiganaji wa kigeni. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya shughuli za kurekebisha na kurejesha jamaa tena kwenye jamii.

| ENEO LA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Ushauri Nasaha, Kupona Kutokana na Tamauko, na Usaidizi kuhusu Tamauko | Kuwarejesha wapiganaji wa kigeni, pamoja na familia zao, mara kwa mara kunaweza kukabiliwa na tamauko ya kimwili au kimawazo. Katika hali hizi, huduma za ushauri nasaha pamoja na usaidizi maalum kuhusu tamauko zinaweza kuwasaidia kuyachanganua matukio ya zamani na kujumuika tena katika jamii. | Mpango wa Kumekucha ulianzishwa na Green String Network nchini Kenya, mpango unaoongozwa na jamii wa kuleta umoja. Kumekucha ni mbinu halisi, ambayo inazungumzia dhana muhimu ya tamauko, ikijumuisha athari za tamauko, njia za kukabiliana nayo, msamaha, kupona, upatanisho, ustahimilivu, na kushughulika na matukio ya nyuma. Shirika hili linajumuisha hadithi za kitamaduni na sanaa kutoka nchini Kenya, ambazo huonyesha muktadha sahihi wa kuelewa tamauko na uponyaji.<br><br>*Mahitaji mengine na /au programu kuhusu usaidizi wa ushauri nasaha na tamauko.*<br>• Jinsi ya Kuwarekebisha na Kuwarejesha Wanamgambo wa Kivita katika jamii: Kushughulikia Tamauko na Kupunguza Unyanyapaa (USIP)<br>• Vijana, Masumbuko na Itikadi Kali (Siku zijazo zisizo na Vurugu)<br>• Masumbuko kama chanzo cha Itikadi kali za Kikaktili (START) |

## Mipango ya Ushirikishaji na Uwezeshaji wa vijana

Shughuli za P/VCE zinazolenga vijana zinaweza kuwa na mwonekano tofauti kulingana na muktadha. Kwa kuwa makundi yenye itikadi kali mara nyingi hujaribu kuajiri vijana walionyimwa haki zao na kuwachochea kufanya vitendo vya kikatili, mipango nyingi ya P/CVE inaangazia vichochezi vinavyoambatana na kutoshirikishwa kwa vijana na ukosefu wa ushirikiano katika jamii zao. Shughuli za kuingilia kati zenye ufanisi mara nyingi hushirikisha vijana moja kwa moja katika upangaji wa shughuli za P/CVE. Kwa kuwawezesha vijana na kuwafanya mawakala wa mabadiliko ndani ya jamii zao wenyewe, uwezekano wao wa kuwa na msimamo mkali wa itikadi kali unaweza kupungua. Ifuatayo ni mifano ya baadhi za shughuli za P/CVE zinazoongozwa na vijana.

| ENEO LA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Uwezeshaji wa Vijana kwa Jumla | Mojawapo wa njia ya kuwawezesha vijana ni kuwapa mafunzo, maarifa na ujuzi ili kuwafanya wenye kuleta mabadiliko katika jamii zao wenyewe. Vijana wanaohisi kutokuwa na uwezo na hawawezi kuleta mabadiliko wanaweza kusababisha kunyimwa haki na kutengwa, jambo linaloweza kupeleka kujiunga na makundi ya itikadi kali. Hata hivyo kupitia kwa shughuli maalum, vijana wanaweza kupewa ujuzi ili wajihisi kuwa muhimu na wenye ushawishi kwenye jamii zao. | Mpango wa Kuzuia Itikadi Kali za Kikatili Kupitia kwa Kuwawezesha Vijana nchini Jordan, Libya, Morocco na Tunisia. unaotekelezwa na UNESCO unatumia mkabala unaojumuisha sekta mbalimbali. Dhamira yake ni kujenga mazingira ambapo vijana wa kike na kiume wanawezeshwa, kusikizwa, na kuhusishwa kama wenye kuleta mabadiliko katika jamii zao ili kuzuia itikadi kali kwa: (1) kKuwafunza vijana maadili, mitazamo, maarifa na ujuzi; (2) kukuza mabadilishano wa mawazo, mawasiliano na ushirikiano zaidi ya mipaka ya kijamii, kiutamaduni na kiisimu; (3) kusaidia ushiriki wa kiraia wa vijana; (4) kuhimiza ushirikiano katika kuleta amani; na (5) kukuza haki za binadamu na ufahamu wa tamaduni. mbalimbali.<br>*Miradi mingine ya uwezeshaji vijana:*<br>• Yes Youth Can (Mercy Corps-Kenya)<br>• Kuwahusisha Vijana katika Kukabiliana na Itikadi kali za Kikatili nchini Nigeria (IREX) |
| Kuwahusisha Vijana Wasio na Ajira au Walio na Ajira ya Kiwango cha Chini | Katika jamii nyingi, suala la kutokuwa na ujuzi ufaao linazidi kuongezeka katika suala la ukosefu wa ajira kwa vijana. Katika muktadha huu, vijana hawana ujuzi wa vitendo unaohitajika kupata ajira ya maana. Ukosefu huu wa uwezo unaweza kupeleka ukosefu wa haki na kuwafanya vijana kuwa katika hatari ya kujiunga na makundi ya kikatili. Kwa kuwapa vijana ujuzi-vitendo unaowawezesha kupata ajira, uwezekano wa kuathiriwa na itikadi kali unaweza kupungua. | Huko Ufilipino, mpango wa EDC Mindanao Youth for Development (MYDev) hutoa ujuzi wa maisha na mafunzo ya ajira kwa vijana walio katika hatari ya kuajiriwa na vikundi vya vurugu. Mradi huo umeonyesha kwamba kuwa na ujuzi mwafaka ni muhimu sana kwa vijana. Kupitia mpango huo, vijana wanatambulishwa kwa makundi yao, wakufunzi, na viongozi wa jamii ambao wanataka kuleta mabadiliko. Wanajifunza kile wanachoweza kutarajia kutoka kwa serikali na kile wanachopaswa kujifanyia, suala linalowazuia kuhisi kutengwa. Kutokana na ripoti za Jeshi la eneo hilo, makundi yenye misimamo ya itikadi kali yamesitisha uajiri katika baadhi ya miji ambamo MYDev inatoa huduma zao.<br>Mifano mingine:<br>• Shughuli ya Muungano wa Maendeleo ya Vijana nchini DRC (EDC) |
| Ushauri au Watu Wenye tabia nzuri za Kuigwa | Ushauri au mipango ya kuigwa ni njia bora za kuzuia VE. Kwa kuwaunganisha watu waliojitayarisha kuzuia itikadi kali katika jamii zao, viongozi hawa wanachukuliwa kama watu wenye tabia nzuri ya kuigwa na vijana wanaoweza kushawishika kujiunga na misimamo ya itikadi kali. Watu wenye tabia nzuri za kuigwa wanaweza kuwa washauri wa kitamaduni, lakini wanaweza pia kuwa wanarika na vijana wenzao. Watu wa kuigwa pia wanaweza kuwa waliokuwa wafuasi wa itikadi wanaotaka kuzungumza na wale walio katika hatari ya kujiunga na makundi ya kikatili na kueleza waliopitia. | Kuimarisha Ustahimilivu dhidi ya Ukatili wenye Misimamo mikali katika Pembe ya Afrika (STRIVE) inachangia katika kuongeza amani, utulivu na fursa shirikishi za kiuchumi kwa vijana na maeneo yaliyotengwa nchini Kenya kwa kufanya utafiti na shughuli za kupunguza watu wanaojiunga na itikadi kali. Kutoa ushauri kwa vijana ni mojawapo ya vipengele muhimu katika programu ambayo inatoa usaidizi wa rika-kwa-rika kwa vijana walio katika hatari ya kuajiriwa na VEOs. Mpango huu unashirikiana na wenyeji katika kupunguza itikadi kali za vurugu kwa kuongeza ujuzi wao kuhusu sababu mbalimbali za kujihusisha na makundi yenye vurugu na/au yenye msimamo mkali. Makundi yanayolengwa na mpango huu ni vijana kutoka jamii zisizo na upendeleo nchini Kenya ambao wanajishughulisha kama washauri na washauriwa, wakifuatwa na washikadau wa ndani.<br>*Nyenzo muhimu ya Ushauri wa Vijana:*<br>• Mafunzo Yanayotokana na Ushauri wa Vijana wa P/CVE (RUSI) |

| ENEO LA SHUGHULI | MAELEZO | MIFANO YA MIRADI |
|---|---|---|
| Michezo na Sanaa | Kushirikisha vijana katika shughuli za michezo na sanaa ni mifano ya kawaida ya mipango mashuhuri ya P/CVE. Michezo, sanaa, na shughuli nyingine za kitamaduni zinaweza kukuza uaminifu miongoni mwa vijana walio katika mazingira magumu na kutoa mitazamo halisi kwa masuala ya jamii na kisiasa kupitia mazungumzo. Shughuli hizi pia zinaweza kusaidia kuwapa vijana hisia kubwa ya kusudi na heri njema kwa jamii yao. | Mnamo Januari 2017, Search for Common Ground ilizindua Mpango wa Kuimarisha Ustahimilivu na Ushirikiano wa Vijana Kupitia Vitabu vya Katuni, mradi wa majaribio wa kujenga ujasiri dhidi ya itikadi kali za kikatili miongoni mwa vijana nchini Tunisia. Mradi huo ulilenga kuwapa vijana ujuzi wa kuunda katuni kama njia mbadala ya kukabiliana na ujumbe unaohimiza vurugu. Mradi huo ulifanya vijana wa Tunisia wawe na sauti. Vijana hao walikuwa na njia chache za kujadili masuala nyeti kama vile itikadi kali. Wengi walipendekeza kubadilisha kitabu cha katuni kuwa msururu wa vipindi, au kufanya maudhui kuwa dijitali na kuwekwa kwa mitandao ya kijamii. Mradi huu ulitoa nakala 4,500 za kitabu cha katuni kinachoitwa Youmiyyat Daly (Siku Katika Maisha ya Daly).<br>Mifano mingine:<br>• Michezo na Usalama (Umoja wa Mataifa) |
| Usimulizi wa hadithi | Kuwahusisha vijana kupitia kusimulia hadithi kunaweza kuzibua nafasi nzuri na salama kwa vijana kujieleza, kuimarisha ustadi wa kujieleza, kukuza uhusiano wa kijamii, na huruma - zote ni mbinu muhimu za kuzuia vurugu. Kupitia kwa kusimulia hadithi, vijana wanaweza kueleza mawazo na hisia zao kuhusu mada kama vile vurugu na itikadi kali. | Katika mataifa kama Jordan na Indonesia, Search for Common Ground hutekeleza mipango ambapo vijana wanapewa ujuzi wa kutengeneza filamu fupi kuhusu maisha yao, migogoro yao na matarajio yao. Kwa kusimulia hadithi zao na kutumia filamu katika maonyesho ya umma na kufanikisha mijadala, vijana wanaweza kuhisi kuwa muhimu na wenye nguvu katika jamii zao. Kupitia kwa kusimulia hadithi, vijana wanaweza kuondoa mgawanyiko, kushirikisha mamlaka ya nchini, na kuwezesha mazungumzo na utatuzi wa matatizo kwa ushirikiano. |